**Fahamu kuhusu Malaika.**

Malaika ni viumbe wa kiroho walioumbwa na Mungu mahsusi kabisa kwa huduma za mbinguni na duniani. Hii ni katika ulimwengu wa sasa na pia katika ulimwengu wa milele ule ujao.

**Biblia inasema,**

*Je! Yuko malaika aliyemwambia wakati wo wote, Uketi mkono wangu wa kuume Hata nitakapoweka adui zako chini ya nyayo zako? Je! Hao wote si roho watumikao, wakitumwa kuwahudumu wale watakaourithi wokovu?* (Wabrania 1:13.14)

Hivyo, Malaika ni roho wanaotumika na kutumwa ili kuwahudumia waurithio wokovu. Kila mwanadamu anatakiwa kuwa mrithi wa wokovu, uliopatikana kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kabla na baada ya Adamu na Eva kutenda dhambi pale bustani ya Edeni. Katika Biblia, tangu uumbaji wa Mungu, Malaika wameonekana wakitumwa na Mungu kuja duniani kuhudumu, au kuleta taarifa kuhusu mambo mbalimbali ambayo Mungu alitaka yafahamike au yasifanyike.

Watu wa Mungu, Nuhu, Ibrahimu, Isaka, Yakobo, Lutu, Musa na wengine wengi, walikutana na Malaika na kupokea jumbe mbalimbali. Hata Samsoni kabla hajazaliwa, mama yake alipokea mwongozo kutoka kwa Malaika kwamba, atazaa mtoto wa kiume ambaye ni Samsoni.

Biblia inasema, *Palikuwa na mtu mmoja wa Sora, wa jamaa ya Wadani; jina lake akiitwa Manoa; na mkewe alikuwa tasa, hakuzaa watoto.Malaika wa Bwana akamtokea yule mwanamke, akamwambia, Tazama, wewe sasa u tasa, huzai; lakini utachukua mimba, nawe utamzaa mtoto mwanamume.* (Waamuzi 13:2.3)

Malaika wapo wengi, lakini Biblia inamtaja mara kwa mara Malaika Gabrieli, ambaye ni Afisa Habari wa Mungu. Pia Biblia inamtaja Malaika Mikaeli kama Mkuu wa Majeshi ya mbinguni.

Na Malaika hao wakati wa kuwasilisha taarifa, wamekuwa wakizitoa hizo taarifa kama wao ndio watendaji, ili kuleta karibu kazi ya Mungu kwa wanadamu’

Biblia inasema hivi,

*Malaika akamjibu akamwambia, Mimi ni Gabrieli, nisimamaye mbele za Mungu; nami nimetumwa niseme nawe, na kukupasha habari hizi njema. Na tazama! Utakuwa bubu, usiweze kusema, mpaka siku ile yatakapotukia hayo, kwa sababu hukuyasadiki maneno yangu; nayo yatatimizwa kwa wakati wake.* (Luka 1:19.20)

Baadhi ya watu hudai kwamba, Malaika wameumbwa kwa moto. Na wengine huwafananisha Malaika na wanawake wazuri au watoto wachanga. Na hii ni kutokana na ukweli kwamba, hakuna binadamu aliyeliona umbo halisi la Malaika, bali tunaamini kupitia Biblia kwamba, Mwenyezi Mungu aliumba viumbe vinavyoonekana na visivyoonekana.

Ukipitia maandiko mbalimbali, Mungu katika uumbaji wake, utaona Malaika waliumbwa na Mungu. Kisha tena, tunaona kwamba hao Malaika hawazai wala hawazaliwi.

Lakini vilevile, kupitia maandiko hayo, hayo, katika Biblia, tunaona kuwa, Malaika anapotumwa kwa binaadamu hutokea kwa umbo la binadamu.

*Basi ikawa, alipokuwa akifanya kazi ya ukuhani katika taratibu ya zamu yake mbele za Mungu, kama ilivyokuwa desturi ya ukuhani, kura ilimwangukia kuingia katika hekalu la Bwana ili kufukiza uvumba.Na makutano yote ya watu walikuwa wakisali nje saa ya kufukiza uvumba.Akatokewa na malaika wa Bwana, amesimama upande wa kuume wa madhabahu ya kufukizia.* (Luka 1;8.11)

Ukipitia maandiko ya hapo juu, kuhusu umbo halisi la Malaika, utagundua kuwa, wamefananishwa na vitu vizuri vinavyovutia machoni pa binadamu, lakini ni ukweli usiopingika kwamba, Malaika hawajaumbwa kwa mfano wa Mungu kama ilivyo kwetu sisi wanadamu.

Biblia inasema,

*Mungu akasema, natumfanye mtu kwa mfano wetu, na kwa sura yetu*…. (Mwanzo 1:26.28)

Lakini kwa haraka twaweza kusema kuwa Malaika ni wanaume, kwani pale wanapojitokeza mbele ya wanadamu, hasa inatokana na tafsiri halisi ya majina yao sio ya kike bali ni ya kiume, kama vile, Gabrieli, au Mikaeli, au Malaika Rafaeli.

Pia katika Biblia kitabu cha Mwanzo, Malaika walipofika nyumbani kwa Lutu, wanaume wa Sodoma walimfuata Lutu wakimwambia awatoe hao Malaika ili

wawajue (wawaingilie kimwili). Na tunajua kuwa, dhambi kubwa ya watu wa Sodoma na Gomola kwa wakati ule, ilikuwa ni ulawiti.

Pia ieleweke vizuri kwamba, Malaika hawana mawazo binafsi au utashi wao binafsi, bali wanaongozwa na maagizo ya Mungu mwenyewe muda wote.

Malaika akamjibu akamwambia*, Mimi ni Gabrieli, nisimamaye mbele za Mungu; nami nimetumwa niseme nawe, na kukupasha habari hizi njema.* (Luka 1:18)

Katika lugha nyepesi tunaweza kusema, Malaika ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu ambaye Mungu mwenyewe humtuma sehemu yoyote kusaidia wanadamu au kufikisha ujumbe wa Mungu kwa wanadamu.

Je! Binadamu anayefikisha ujumbe wa Mungu pia tunaweza kumwita ni Malaika? La hasha! Huduma alizozitoa Mungu kwa wanadamu ni tano tu ambazo ni, **Utume, Unabii, Uinjilisti, Uchungaji na Ualimu.** Kwa kusema hivi naweza kusisitiza kuwa sio sahihi hata kidogo mjumbe wa Mungu yaani mtu kama mimi na wewe aliyeumbwa kwa udongo kumwita eti yeye naye ni Malaika, kwa sababu tu anafikisha ujumbe wa Mungu. Lakini akiitwa Mtume, Nabii, Mwinjilisti au Mchungaji na Mwalimu hakutakuwa na makosa, kwani ndivyo ilivyo. Ni vema kila kitu kitumike mahala pake.

SAUTI ZA MALAIKA

Mara zote limekuwa ni jambo la kufikirika kwamba, je! Malaika wana lugha na namna ya milio ya sauti zao ipoje? Ni kweli kuwa, Malaika wana lugha za kimbingu, maana hao hutenda kazi zao kwa agizo la Mungu, ambaye ndiye Neno kama Paulo alivyosema kwamba,

Nijaposema kwa lugha za wanadamu na Malaika kama sina upendo si kitu mimi……(1 Wakorintho 13:1)

Maneno ya Paulo yanatoa udhihirisho wa uwepo wa lugha za Malaika. Japokuwa mara zote Malaika wamekuwa wakiwasiliana na binaadamu kwa lugha za kibinadamu, kwa ufupi kabisa.

Kwa mfano:

ONDOKA UPESI

Maneno haya aliambiwa Petro alipokuwa gerezani.

Biblia inasema,

*Mara malaika wa Bwana akasimama karibu naye, nuru ikamulika mle chumbani, akampiga Petro ubavuni, akamwamsha, akisema,* ***Ondoka upesi****. Minyororo yake ikamwanguka mikononi.* (Matendo ya Mitume 12:7)

Ukifuatilia kwa makini hayo mazungumzo ya Malaika, utabaini kwamba, maneno yao huyatamka kutokana na maagizo waliyopewa. Hawaongezi wala hawapunguzi.

Katika Biblia, kitabu cha Ufunuo kinaeleza kwa kina sana juu ya dhana hii ya sauti za Malaika, hivyo ukweli ni kwamba, Malaika wana lugha na wanazungumza lugha yoyote ile kulingana na ni nani wanayemhudumia na kwa jambo gani.

Katika miaka ya hivi karibuni, wanasayansi kutoka mataifa makubwa duniani wameanza kukutana na nguvu za Malaika na kwa sababu hawakubali moja kwa moja juu ya uwepo wao, wameamua kuwaita UFO au viumbe wasioonekana wanaoishi angani. Ni ukweli kwamba, wanasadiki juu ya uwezo wao wa ajabu na mkuu sana. ‘